Toleo 11

# Ukweli wa Injili

*Mafundisho ya Biblia na Himizo kwa Kazi ya Kimisheni Ulimwenguni Kote*

## NI NANI MKUU ZAIDI

Yesu na wanafunzi wake walikuwa wakitembea kwenye barabara iliyojaa vumbi ya kuelekea huko Kapernaumu. Lakini wanafunzi hao walionekana kupunguza mwendo sana. Punde si punde wakaanza kuachwa nyuma na Yesu kwa sababu walianza kubishana kuhusu "ni nani kati yao alikuwa mkuu Zaidi?" (Marko 9:43b).

Maono yao yalikuwa kwamba kabla ya muda mwingi kupita Israeli wangeweza kupata uhuru kutoka kwa utawala wa Ufalme wa Kirumi na wanafunzi hao wangeanza kuitawala Israeli pamoja na Masihi, wao wakiwa kama wafalme na wana wa kifalme. Kufikia wakati huu wao hawakuwa wameelewa kwamba ufalme wa Mungu haukuwa wa kisiasa, ya kwamba ulikuwa ufalme wa kiroho (Luka 17:21; Warumi 14:17).

Mgogoro wao ulizidi kuwa mkali zaidi walipokuwa wakishughulikia swala la ni nani kati yao alistahli kuwa na heshima na cheo kikubwa zaidi katika ufalme wa Yesu. Mmoja wao akasema, "Bila shaka mimi ndiye ninastahili kuwa mkuu zaidi, mimi ndiye mzee kuliko nyinyi nyote!"

Lakini mwingine akamjibu, "Hapana! Mimi ndiye ninastahili cheo kikuu zaidi, mimi nina ujuzi zaidi wa kutatua matatizo ya watu – hebu tazama mvi zilivyo nyingi kichwani mwangu."



Naye mwingine akasema yafuatayo (huku sauti yake ikiwa ya mtu mwenye chembechembe za hasira), "La, hasha! Nyinyi nyote mmekosea. Mimi ndimi mwenye elimu nyingi zaidi, mwenye uwezo zaidi, na mwenye hekima kuliko nyinyi nyote wawili."

Mwingine akasema, "Acheni hayo yote, mimi ndimi nimekuwa na Yesu kwa muda mrefu zaidi. Nilikuwa wa kwanza kuanza kumfuata."

Hapo ndipo walianza kupaza sauti kutokana na hasira na kuhisi uchovu wa majibizano yao; kila mmoja akijaribu kutetea haki yake ya kuwa mkuu zaidi. Hakuna hata mmoja kati yao alitaka mwanafunzi mwingine yeyote kuwa mtawala juu yake. Na katika majibizano hayo mmoja wa wanafunzi hao akasema bila wasiwasi wowote (lakini kwa uamuzi wa kumaanisha kabisa kutoka moyoni mwake): "Mimi ndimi nitakuwa mkuu zaidi, jamii yangu ndio ambayo inaheshimika zaidi katika taifa lote la Israeli."

Walakini, hapo baadaye Yesu akawauliza wanafunzi wake, "Mlishindania nini njiani?" (Marko 9;33; tazama pia Luka 22:24).

Ndipo Yesu akaanza kuwafundisha wanafunzi wake kuhusu ukuu ulio wa kweli, huku akifahamu mitazamo ya kimwili na ya kiburi ambayo ilikuwa mioyoni mwao. Akamwita mtoto mdogo na kumsimamisha katikati yao na kuwaambia, "Basi, ye yote ajinyenyekeshaye mwenyewe kama mtoto huyu, huyo ndiye aliye mkuu katika ufalme wa mbinguni" (Mathayo 18:4). "Mtu atakaye

*(Inaendelea kutoka ukurasa 2)*


Tahariri 3

Kujifunza Biblia: Kuoshana Miguu 4

Nakala ya Kuandamana na Mafunzo ya Biblia 5-6

Maswali na majibu: 7

Je Wajua?

Neno Linalofaa kwa Msimu Huu 8

MAMBO AMBAYO

# BIBLIA

## Inafundisha Kuhusu...

**Neno la Mungu**
2 Tim. 3:6, 2 Pet. 1:20-21, Mt. 24:35
**Uhusiano wa Upendo**
Mt. 22:37-40, Yn. 14:21-23, 1 Yoh. 4:7-21
**Toba**
Mdo. 3:19, 17:30, 2 Kor. 7:10
**Uzao Mpya**
Yn. 3:3-7, 2 Kor. 5:17, Rum. 6:1-4, Efe. 2:1, 5-6
**Uhuru Kutokana na Dhambi**
1 Yoh. 5:18, Mt. 1:21, Yn. 8:11
**Ujazo wa Roho Mtakatifu**
Mdo. 19:2, 15:8-9, 1:8
**Utakatifu**
Lk. 1:73-75, Ebr. 12:14, 1 Pet. 1:15-16, Tit. 2:11-12, Rum. 6:22
**Ufalme wa Mungu**
Lk. 17:20-21, Rum. 14:17, Yn. 18:36
**Kanisa**
Mdo. 2:47, Efe. 4:4-6, 1 Kor. 12:12-13, Kol. 1:18
**Umoja**
Yn. 17:20-23, Gal. 3:28, Ufu. 18:2-4
**Kanuni za Kanisa**
Mt. 28:19-20, 26:26-30, I Kor. 11:23-27, Yn. 13:14-17
**Uponyaji wa Kiungu**
Lk. 4:18, Isa. 53:4-5, Yak. 5:13-16
**Utakatifu wa Ndoa**
Mt. 19:5-6, Lk. 16:18, Rum. 7:2-3, I Kor. 7:10-11
**Urembo wa Nje**
I Tim. 2:9-10, I Kor. 11:14-15, Kum. 22:5
**Mwisho wa Nyakati**
2 Pet. 3:7-12, Yn 5:28-29, 2 Kor. 5:10, Mt. 25:31-46
**Kupenda Amani**
Lk. 6:27-29, 18:20
**Ibada**
Yn. 4:23-24, Efe. 5:19, 2 Kor. 3:17
**Wajibu Mkuu**
Mk. 16:15

*(Endelea kutoka ukurasa 1)*

kuwa wa kwanza atakuwa wa mwisho kuliko wote, na mtumishi wa wote" (Marko 9:35b). "Akawaambia, Wafalme wa Mataifa huwatawala, na wenye mamlaka juu yao huitwa Wenye fadhili;  lakini kwenu ninyi sivyo; bali aliye mkubwa kwenu na awe kama aliye mdogo; na mwenye kuongoza kama yule atumikaye" (Luka 22:25-26).

Kiburi ama mtu kujitakia cheo kwa kutumia njia za kimwili ni mambo ambayo hayana nafasi kati ya watu wa Mungu. Katika ulimwengu wa kidini wahudumu wengi wa Injili hukazana ili kuonekane kwamba wamepata vyeo vilivyotukuzwa, vyenye nguvu na vyenye kutambulika. Wao huwa na shauku la kuwa wakuu zaidi ili watu wale wengine wanyenyekee kwao na kuwatii. Shauku lao huwa ni kutawala kama mabwana na machifu wenye vyeo vikuu katika makusanyiko ya watu wa Mungu na hata kati ya wahudumu wenzao wa Injili. Nao Wakristo wengi walio-okoka na wahudumu wa Injili hujaribu kuwalazimisha watu wale wengine wawapatie heshima na mamlaka kutokana na umri wao, ujuzi wao, elimu yao, familia zao, au kutokana na vyeo vyao. Lakini Bwnaa Yesu alifundisha na pia Yeye alikuwa mfano wa kitu ambacho ni tofauti kabisa. Yeye alidhihirisha ukuu wa kweli kupitia kwa roho ya unyenyekevu na roho wa kuwatumikia watu wale wengine. Ni nani ambaye ni mkuu zaidi? Ni mwanamke au mwanaume ambaye hunyenyekea kama mtoto mdogo na kuwatumikia watu wale wengine kwa upendo na kunyenyekea bila kiburi. Ukuu wa kweli haupatikani katika utawala mbali hupatikana kwa mtu kuwa na roho ya utumishi. Huyu ndiye roho ambaye hajitukuzi, ila lengo lake ni kuwajenga watu wale wengine. Ni ombi letu kwamba kila mtoto wa Mungu na kila mhudumu wa Injili atajua ukuu ulio wa kweli.

--mws


### UKWELI WA INJILI

Gazeti la '*Ukweli wa Injili*' huchapishwa kwa jina la Bwana kwa matumizi ya watu wa mataifa yote kwa kusudi la kuimarisha na kuwahimiza watu wote katika ukweli wa neno la Mungu. Gazeti hili hufundisha na kueneza ukweli wa Biblia ambao umethibitishwa tangu nyakati za Yesu Kristo na mitume.

Neno la Mungu ndio mwongozo halisi na wa kipekee wa imani. Linafundisha wokovu na ukombozi kutokana na dhambi unaoletwa na utakaso wa Yesu Kristo; ambao hufuatiwa na ujazo wa Roho Mtakatifu anayemwongoza mhudumu, kumwonyesha njia, na kumpatia nguvu; pia unamletea mtu utakatifu halisi katika kila fani ya maisha yake; na pia kuleta umoja na utangamano wa watu wa Mungu. Huduma inayokubalika na Mungu inatokana na mtu kuwa na uhusiano wa kibinafsi na wa upendo ambao msingi wake ni ukweli.

Waandishi: Michael na René Smith

### UAGIZAJI

*Ukweli wa Injili* ni gazeti la kieletroniki linalochapishwa kila robo ya mwaka jinsi mungu anavyotuongoza. Tutembelee katika tovuti yetu ya www.thegospeltruth.org ili uagize jalida hili kupitia kwa orodha yetu ya anwani pepe na upokee toleo lako la wakati huu. Hebu jisikie huru kututumia orodha ya majina na anwani pepe za watu wengine ambao wangependa kupokea toleo hili kutoka kwa mwandishi wa jalida la Ukweli wa Injili.

### WASILIANA NASI

Gazeti a *Ukweli wa Injili* linachapishwa katika mataifa mbalimbali ili kusambazwa katika maeneo hayo. Kazi hii na zingine za kimishenari ambazo sisi hufanya huwezekana kupitia kwa matoleo ya kujitolea yanayotolewa kwa jina la Kanisa la Mungu.



Ukweli wa Injili, 605 Bishops Ct., Nixa, MO 65714 USA
editor@thegospeltruth.us

# Tahariri



*Nikimtumikia Bwana kwa unyenyekevu wote….*– Matendo 20:19a.

Mimi namshukuru Mungu kwa kunipa nafasi ya kujua Wakristo walio watakatifu, ambao walikuwa nguzo la kanisa, na ambao walinipatia mfano mzuri wa unyenyekevu ulio wa kweli katika huduma ya Bwana. Kizazi hiki tunachoishi huongozwa na watu kuzitakia nafsi zao makuu, watu wenye kiburi ambao malengo na maono yao huongozwa na tamaa za mwili. Jambo hili huwa kweli hata katika ulimwengu wa kidini, ambako wahudumu wengi ni watu walio kiburi na ambao malengo yao ni kujifaidi wenyewe. Ni jambo mbaya sana kuona watu waliojitangaza kuwa wahudumu wa Injili wakikazana kupata vyeo na heshima za kibinadamu, huku pia wakiwa na wivu wa kuona jinsi wahudumu wengine wa Injili walivyonawili katika mambo ya kiroho.

Lakini pia ni jambo la kufurahisha kuona watu wanaomtumikia Bwana kwa unyenyekevu WOTE wa moyo. Ni jambo la baraka kuu kuona kwamba katika Kanisa la Mungu kuna watu ambao wanafuata mfano wa Bwana wao wa kuwa na unyenyekevu kutoka moyoni mwao. Mahali ambako kuna mvutano na ugomvi hapo pia utapata roho ya kimwili na yenye kiburi ikijidhihirisha. Unyenyekevu ni jambo muhimu sana na ndilo jambo linalodhihirisha wahudumu wa kweli wa Injili.

Katika robo hii ya mwaka tumejifunza kuhusu kanuni ya kuoshana miguu na mambo ambayo tunaweza kujifunza kutokana na kanuni hiyo. Ni jambo la baraka kubwa mtu kuwa kati ya watu wacha Mungu ambao wanaamini na kufuata tamaduni hii na ambao ni wanyenyekevu na kufikia hata kukubali kuoshana miguu. Kwa kweli tendo la kimwili la kuoshana miguu halimvutii mwanadamu, lakini baraka za kiroho ambazo huletwa na tendo hilo ni za ajabu.

Katika maisha haya watu wanaweza kufikia ambapo hawaelewani na kunaweza kuwa na matatizo ya mahusiano kwa sababu ya tofauti zao za kimaumbile na za mielekeo tofauti ya watu. Lakini roho ya unyenyekevu itasuluhisha mengi ya matatizo yanayozuka kati ya mtu na mwenzake. Sifa hizo za unyenyekevu ndizo ambazo mtu anahitaji ili aweze kusema "Mimi ndimi mkosaji," au aseme, "naomba msamaha." Hata tukijihisi kwamba sisi ndio wenye haki ni jambo muhimu sana kwa sisi kuwa na unyenyekevu moyoni. Wakati kanisa au ndugu wanakuwa na shida huo ndio wakati bora kwa wao kufanya kanuni hiyo ya kuoshana miguu na kumtamfuta Mwenyezi Mungu ili awapatie unyenyekevu wa hali ya juu.

Lakini kuna watu ambao hudai mtu fulani amekosa unyenyekevu kwa sababu yeye amesimama kidete kwa mambo ambayo anaamini. Mara nyingi watu ambao husimamia uongozi husemekana kwamba wana kiburi kutokana na matendo yao ambayo sana sana huhusiana na vyeo ambavyo wameshikilia. Basi tunahitaji kuwa waangalifu ili tusiseme kwamba watu wa Mungu wana kiburi kwa sababu wanaonekana sana hapo jukwaani kutokana na wadhifa ambao wameshikilia.

Mimi ninakumbuka miaka kadhaa iliyopita wakati nilipokuwa nikifundisha kundi la wachungaji kuhusu mfano wa Kristo wa unyenyekevu na utumishi. Wao hawakufurahishwa na mafundisho yangu kwa sababu yalikuwa kinyume na shauku yao ya kufanya huduma inayowainua juu ya watu wale wengine kanisani. Lakini mambo hayastahili kuwa hivyo kati ya wa watu wa Mungu. Lengo letu na wito wetu ni kuwa na moyo na nia ya utumishi na kuishi maisha ya unyenyekevu.

Hebu basi tumtafute bwana wetu ili tuweze kupata na kudhihirisha roho ya unyenyekevu katika kila hali, jambo ambalo ndilo lilikuwa shauku kubwa la Yesu wakati Yeye alianzisha kanuni ya Wakristo kuoshana miguu.

Michael W. Smith

Januari 2015

mengi kwa

MTANDAO

*Tutembelee kwa*

*www.thegospeltruth.org*

*ili uagize na kusoma*

*jarida letu.*



# Nyinyi Nyote ni NDUGU

(Mathayo 23:1-12)

Mafarisayo walipenda kutukuzwa na kuheshimiwa na wanadamu. Furaha yao ilikuwa ni ule utukufu na vyeo vyao. Lakini Yesu aliwaagiza wanafunzi wake wasiitwe Rabi, Baba, Mkubwa, au Kiongozi. Kristo ndiye kiongozi na mkubwa wetu, na Mungu ndiye baba wetu wa kiroho ambaye yumo mbinguni.

Wakati wahudumu wa Injli wanafanya kazi ya nyadhifa mbali mbali katika mwili wa Kristo wao hawastahili kuchukulia kuwa wamepanda vyeo (eti wao ni Baba, Bwana, Askofu, Kasisi, n.k.).

Huduma katika kanisa la Agano Jipya haina uhusiano wa mkubwa kwa mdogo. Badala yake kunao usawa kati ya wahudumu wa Injili. Kwa maneno yake Kristo, "Sisi sote ni ndugu."

# MWONGOZO WA KUJIFUNZA BIBLIA

## Somo: KANUNI KUHUSU WAKRISTO KUOSHANA MIGUU

**Somo la Biblia:** Basi, ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu nimewaosha nyinyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuoshana miguu – (Johana 13:14 BHN).

**Muhstasari:** Yesu Kristo ndiye alianzisha kanuni ya Wakristo kuoshana miguu. Wakristo wote wameagizwa kufuata mfano huo wake. Watakatifu wa Mungu wameitwa ili wawe watumishi. Tendo hilo la kuoshana miguu ni ukumbusho kuhusu usawa na unyenyekevu ambao unastahili kuweko milele katika mwili wa Kristo (soma Yohana 13:1-17).

**I. Ulianzishwa na Kristo**

Yohana 13:1-5 Yesu aliosha miguu ya wanafunzi wake.

**II. Iliamrishwa na Kristo**

A. Mathayo 28:20 Mfuate mambo yote.

B. Yohana 13:14 Mnapaswa . . .

1. Paswa: Mtu kuwa na deni, jambo la lazima, wajibu ambao ni lazima mtu atimize.
2. Tazama Luka 18:1; Matendo 5:29; 1 Yohana 4:11.

**III. Mfano Mkamilifu ni wa Kristo**

Yohana 13:15 Mfano wa Kristo.

**IV. Ni Jambo Ambalo Lilifanywa Katika Kanisa la Mitume**

A. Yohana 13:8 Ushirika na Kristo.

B. I Timothy 5:9-10 Wajane.

**V. Somo Kuhusu Unyenyekevu**

A. Yohana 13:16 Mtumishi sio mkuu kulio bwana wake.

B. Wafilipi 2:3-7 Nia ya Kristo.

C. Mathayo 18:1-4 Muwe kama watoto wadogo.

D. 1 Petro 5:3-5 Vazi la unyenyekevu.

**VI. Wito wa kuwa Watumishi**

A. Luka 22:24-27 Mtu mkuu kuwa kama mtumishi.

B. Wagalatia 5:13 Tumikianeni mmoja kwa mwingine.

**VII. Somo Kuhusu Usawa**

A. Mathayo 23:8-12 Wote mu ndugu.

B. Wagalatia 3:28 Umoja ndani ya Kristo.

**VIII. Heri Anayopata Yule Ambaye ni Mtiifu**

A. Yohana 13:17 Heri ya kutenda.

B. Isaya 1:19 Mtu kuweza kula mema ya nchi.

***Tamati:*** *Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu; ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa – Wafilipi 2:5-7*



# KANUNI YA WAKRISTO KUOSHANA MIGUU

*Nakala ya kuandamana na mafunzo ya Biblia*

### Hadithi Kulingana na Inavyopatikana Katika Biblia

(Yohana 13:1-17) Yesu akainuka kutoka hapo mezani na akawatazama wanafunzi wake ambao wote walikuwa wamekusanyika hapo. Tayari sasa walikuwa wamemaliza kula chakula cha jioni, chakula cha Pasaka. Yeye alijua kwamba baada ya masaa kidogo angejitoa kama dhabihu pale msalabani kwa ajili ya wokovu wa ulimwengu. Lakini sasa akiwa kama mtumishi alianza kuosha miguu ya wanafunzi wake na kupanguza miguu yao na kitambaa. Baada ya kuosha miguu ya mmoja wa wanafunzi hao alifulululiza hadi kwake Yuda, akamtazama, na huku akijua kwamba punde si punde mwanafunzi huyu angemsaliti, kwa upendo na unyenyekevu akainama mbele ya msaliti huyu wake na kuanza kumwosha miguu.



### Petro Anajihisi Kwamba Hafai

Basi, akamfikia Simoni Petro; naye Petro akasema, "Bwana, wewe utaniosha miguu mimi?" Yesu akamjibu, "Huelewi sasa ninachofanya lakini utaelewa baadaye."

*"Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo."*

Petro akamwambia, "Wewe hutaniosha miguu kamwe!"

Yesu akamjibu, "Nisipokuosha hutakuwa na uhusiano nami tena."

Simoni Petro akamjibu, "Bwana, nioshe, si miguu tu, bali na mikono yangu na kichwa pia."

### Umuhimu wa wakristo kuoshana miguu

Alipokwisha kuwaosha miguu na kuvaa vazi lake tena Yesu akaketi mezani, akawaambia, "Je, mmeelewa hayo niliyowatendeeni? Nyinyi mwaniita Mwalimu na Bwana, nanyi mwasema vyema, kwa kuwa ndimi. Basi, ikiwa mimi niliye Bwana na Mwalimu nimewaosha nyinyi miguu, nanyi pia mnapaswa kuoshana miguu. Nimewapeni mfano, ili nanyi pia mfanye kama nilivyowafanyieni. Kweli nawaambieni, mtumishi si mkuu kuliko bwana wake, wala mtume si mkuu kuliko yule aliyemtuma" (Yohana 13:13-16 BHN).

### Ni jambo lililo Zaidi ya utamaduni

Katika nyakati za Biblia watu kuoshana miguu lilikuwa jambo la kawaida kabisa. Hii ni kwa sababu barabara za wakati huo zilijaa vumbi. Walakini, angalau jukumu la kuosha wageni miguu lilikuwa la watumishi wa nyumbani. Lakini Yesu hakuosha miguu ya wanafunzi ili kuwatoa vumbi. Ni dhahiri kwamba Yesu hakuwa amefanya kitendo kama hicho hapo mbeleni, jambo ambalo ni dhahiri kutokana na mshangao ambao ulimkumba Petro. Yesu alikuwa akifanya jambo ambalo lilikuwa zaidi ya mazoea ya utamaduni. Hii ndio sababu Yesu akamwambia Petro, "Yesu akajibu, akamwambia, Nifanyalo wewe hujui sasa; lakini utalifahamu baadaye" (Yohana 13:7). Basi Yesu alianzisha kanuni ya watu kuoshana miguu ikawa kanuni ambayo Kanisa lilistahili kufuata—tendo la kiroho lililokuwa na maana nyingi sana.

### Kanuni hiyo ilitokana na amri ya kristo

Yesu aliwapatia wanafunzi wajibu wa kufundisha mataifa yote, "Na kuwafundisha kuyashika yote niliyowaamuru ninyi; na tazama, mimi nipo pamoja nanyi siku zote, hata ukamilifu wa dahari" (Mathayo 28:20). Yesu aliweka maagizo kabambe ya jinsi watu wake wanastahili kufuata kanuni hiyo ya kuoashana miguu. Katika lugha ya Kiyunani "neno paswa" lina maana ya: kuwa na deni, kulazimika kufanya jambo, au kuwa na wajibu. "Imewapasa kumwomba Mungu sikuzote" (Luka

*(Endelia kwa ukurasa 6)*

*(Endelea kutoka ukurasa 5)*

18:1b). “Imetupasa kumtii Mungu kuliko wanadamu” (Matendo 5:29b). “Imetupasa na sisi kupendana” (1 John 4:11). Ni dhahiri kwamba watu wa Mungu wana jukumu la kuoashana miguu. Zaidi ya hayo, Yesu alinema kwa njia ya wazi kabisa na kusema, “Kwa kuwa nimewapa kielelezo; ili kama mimi nilivyowatendea, nanyi mtende vivyo.”

### Ilikuwa ni mazoea ya kanisa la kwanza kuoshana miguu

Ingawa makanisa mengi huadhimisha kanuni ya Meza ya Bwana, kanuni ya kuoshana miguu haifanywi na makanisa mengi. Watu wengi hawako tayari kuosha miguu ya watu wale wengine, nao hujaribu kutoa vijisababu vya kutofanya hivyo kwa kujaribu kusema kwamba hawajafanya makosa kwa kutotimiza kanuni hiyo. Lakini kanuni ya kuoshana miguu haikufundishwa tu na Kristo mbali pia ilifuatwa na kanisa la mitume. Wakati kanisa lilipokuwa likimsaidia mjane kwa mambo ya kifedha walichunguza kama mjane huyo alihitimu kupata msaada “ikiwa amewaosha watakatifu miguu” (1 Timotheo 5:10).

### Mfano wa huduma inayoongozwa na unyenyekevu

Bwana Yesu ambaye ni Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana alidhihirisha unyenyekevu na aina ya huduma ambayo inatakikana kuweko kati ya watu wa Mungu, maanake wana wa kweli wa Mungu. Mwokozi wetu hakunyenyekea tu mbele ya wanafunzi wake ambao walimpenda na kumfuata, lakini pia alinyenyekea kwa mwanafunzi ambaye alimsaliti na ambaye alikuwa mnafiki. Roho wa Kristo ni tofauti kabisa na ile roho ya kung’ang’ania vyeo na watu kutaka kufahamika ambayo hupatikana katika ulimwengu wa kidini katika siku hizi tunamoishi. Watu wa Mungu, wahudumu wa Injili, mitume na viongozi wa kanisa sio wakuu kuliko Kristo. Basi sisi sote tunahitaji kufuata mfano wake—badala ya kutaka kuwa mabwana, wakuu, au machifu - tunahitaji kuwa watumishi.

### “Roho” ya kuoshana miguu

“Msitende neno lo lote kwa kushindana wala kwa majivuno; bali kwa unyenyekevu, kila mtu na amhesabu mwenziwe kuwa bora kuliko nafsi yake . . .  Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu;  ambaye . . .



alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa wanadamu” (Wafilipi 2:3-7). Ni tendo la unyenyekevu mtu kuosha miguu ya yule mwingine. Hii ndio roho ambayo Wakristo wanastahili kuwa nayo kila wakati. Wakristo wanastahili kufuata agizo la, “Ninyi nyote jifungeni unyenyekevu, mpate kuhudumiana” (1 Petro 5:5). Hata ikiwa kanuni ya kuoshana miguu haifanywi kila siku, roho ya kuoshana miguu inastahili daima kuweko katika maisha ya Mkristo.

### Kuna heri kwa mtu yule mtiifu

Yesu ndiye alianzisha kanuni ya watu kuoshana miguu kwa njia ya kimwili ili watu wake wapate kuikumbuka roho ya kweli na unyenyekevu, roho ya kutokuwa na ubinafsi, roho ya utumishi, na roho ambayo inawasawazisha watu wote. Basi Yesu akawapatia heri wale ambao ni watiifu, watu ambao wanafuata mfano wake katika mazoea na katika roho “Mkiyajua hayo, heri ninyi mkiyatenda” (Yohana 13:17).

—mws

# MASWALI na MAJIBU

### Je, kanuni ya kuosha miguu inahitaji kufanywa mara ngapi?

Katika Yohana 13 Yesu aliwafundisha wanafunzi wake kwamba walistahili kufuata mfano wake na kufanyiana kile ambacho aliwafanyia. Lakini yeye hakutoa mwongozo wa kwamba kanuni hiyo ifanywe mara ngapi. Kimsingi kanuni huwa ni ishara ya jambo lingine ambalo ni la kiroho. Lakini ikiwa kanuni hiyo itatekelezwa kila siku, kila wiki, au hata kila mwezi inaweza kuanza kupoteza umuhimu wake na kuwa jambo la mazoea tu.

Wengi wa watakatifu walifanya ibada maalum ya kutekeleza kanuni hiii katika mkutano wao wa mwaka. Nayo makusanyiko mengi huwa na mazoea ya kuoshana miguu katika kipindi kile ambacho Pasaka husherehekewa.

Yesu aliosha miguu ya wanafunzi wake wakati wa Pasaka na baada ya hapo ndipo akaanzisha kanuni ya Meza ya Bwana, ama kikombe cha ushirika. Huu basi unakuwa ni wakati wa kukumbuka kifo chake na kusulubiwa kwake. Basi kanuni ya kuoshana miguu wakati mwingi hufanywa katika ibada moja ambako pia ushirika wa Meza ya Bwana unafanywa. Lakini kilicho muhimu zaidi kuliko “ni mara ngapi kanuni ya meza ya Bwana inafanywa?” ni kwamba kanuni hiyo IFANYWE na Wakristo.

### Je, ni jambo linalofaa kwa wanawake na wanaume kuoshana miguu?

Maandiko yamenakili hadithi katika Luka 7:37-39 ambako mwanamke mmoja aliosha miguu ya Yesu kwa kutumia machozi yake. Hata ingawa wale waliojifanya kuwa na utakatifu wa kibinafsi walikilaani kitendo hicho, hiki kilikuwa kitendo maalum cha kumwabudu na kumheshimu Bwana Yesu. Lakini tukio hili halikumaanisha kwamba jambo hilo lifuatwe katika ibada za kawaida za kufanya kanuni hiyo ya kuoshana miguu.

Kuna heshima na vizuizi ambavyo vimo kati ya wake na waume ambazo si jambo la hekima kuzivunja kwa njia ya watu kujifanya wanafanya ibada za kiroho kwenye ibada za kufuata kanuni ya kuoshana miguu. Lakini kunao




utamaduni ambao ni wa kawaida ambako mama mwenye nyumba huosha miguu ya wageni waheshimiwa waliotembea nyumbani mwao, jambo ambalo linafanyika mbele ya washirika wote wa nyumba hiyo. Tamaduni hiyo inafanana sana na tukio hilo ambako mwanamke aliosha miguu ya Bwana Yesu. Lakini tendo hilo la kitamaduni halifananani na tukio ambako Wakristo wanaoshana miguu kwenye ibada za kawaida.

1 Wakorintho 14:40 imenukuliwa kusema, “Mambo yote na yatendeke kwa uzuri na kwa utaratibu,” hata ingawa andiko hilo halizungumzii swala la kuoshana miguu (kwa njia ya moja kwa moja). Katika ile roho ya Wakristo kuwa na kiasi na kufanya mambo yanayofaa katika jamii, andiko hili linafaa sana. Ni jambo la haki na linalofaa kama wanaume na wanawake watatenganishwa wakati kanuni ya uoshaji miguu inafanyika kanisani, na wanaume kuosha miguu ya wanaume wenzao, huku wanawake wakiosha miguu ya wanawake wenzao.

### Je, kwenye ibada ya kuoshana miguu kila mtu anahitaji kuosha miguu ya kila mtu ambaye yuko kwenye ibada hiyo?

Kulingana na mfano wa Yesu, Yeye aliosha miguu ya wanafunzi wake wote. Halafu akawaambia “mnapaswa kuoshana miguu.” Lakini ni jambo ambalo haliwezekani kwa mtu mmoja kuosha miguu ya watu wote ikiwa kikundi hicho kina idadi kubwa ya watu. Umuhimu wa kanuni ya kuoshana miguu ilikuwa kwenye kitendo hicho cha kimwili na cha kiroho cha unyenyekevu cha mtu kupiga magoti na kuosha miguu ya mwenzake.

Ikiwa mtu mmoja ataosha miguu ya mtu mwingine, naye mtu huyo mwingine aoshe miguu ya mwingine, ikiwa wote watafanya hivyo, basi kila mtu atakuwa ameoshana na kila mtu atakuwa ameoshwa. Watu hao watakuwa “wameoshana miguu.” —mws

**JE, WAJUA?**

Kuna ushahidi kwamba kumekuwa na Wakristo ambao walifuata kanuni ya kuoshana miguu katika historia yote ya kanisa. Augustine (ambaye aliishi A.D 400) alikubaliana na tendo hilo la Wakristo kuoshana miguu. Tamaduni hiyo ya kuoshana miguu ilivuma sana huko Uropa ya kusini katika mwaka wa karne ya nne na saba. Nao Wanabaptisti wa karne ya 16 walikuwa wamejitolea kufanya kanuni hiyo kwa mioyo yao yote.

Kuoshana miguu pia ni jambo ambalo lilifanywa katika makanisa mengi ya Kibaptisti huko Marekani hadi hapo mwisho wa karne ya kumi na tisa. Abrahamu Lincoln akiwa kijana mdogo alitayarisha maji ya karae ili Wakristo waweze kutumiza kanuni hiyo ya kuoshana miguu katika kanisa la Kibaptisti huko Indiana ya kusini.

[Brown Charles E. (1947). *Kanisa la mitume*.]

**Neno Linalofaa kwa Msimu Huu**

# Mtumishi wa Kristo

*Paulo, mtumwa wa Kristo Yesu, aliyeitwa kuwa mtume, na kutengwa aihubiri Injili ya Mungu.* —Warumi 1:1

Wahudumu wa kweli wa Injili huitwa na kuwekwa wakfu na Mungu. Wao huwa wamechaguliwa ili kueneza injili na kunena kulingana na wanavyoongozwa na roho. Mtume Paulo alijitambulisha kama "mtumwa wa Kristo." Yeye alikuwa akimtambua Kristo kama Kiongozi na Bwana wake. Kamwe mtume Paulo hakujichukulia kuwa na mamlaka yoyote mbali alifanya kazi yake na kunena kama mtumwa ambaye alikuwa akitimiza mapenzi ya bwana wake.



Wakati ambapo mtumwa/au mtumishi anafuata maagizo ya Bwana sifa za matokeo ya kazi yake hupewa Bwana. Wakati Mungu anabariki na kupaka mafuta juhudi za mhudumu katika ufalme wake, utukufu na heshima zote hutolewa kwa Bwana. Mhudumu mtauwa hastahili kamwe kutukuzwa kutokana na juhudi au kazi zake kwani sote tu watumishi wa Mungu.

Wakati mwingine wahudumu wa injili hufa moyo wakati juhudi zao zinakosa kuzaa matunda mengi. Kuna nyakati ambapo maombi hayajibiwi. Wahudumu wa injili wanaweza kubeba mzigo huo na kujisikia kugandamizwa rohoni kwa sababu ya wao kukosa uwezo wa kubadilisha watu na hali zao. Lakini wewe mtumishi unastahili kuwa na ujasiri na ukumbuke kwamba wewe ni mtumishi tu. Ni nguvu za Mungu na mapenzi yake ndio huleta matokeo katika wakati wake unaofaa na kwa njia zake. Wewe mtumishi wake baki tu ukiwa mnyenyekevu kwake, kuwa mtiifu, kuwa mwaminifu, na umwachie Bwana matokeo ya utumishi wako. Inua kichwa chako na kwa unyenyekevu timiza mapenzi ya Mungu kama mtumishi wa Bwana Yesu Kristo.

—mws

**Anwani**

The Gospel Truth
P. O. Box 2042
Nixa, MO 65714
USA

Email:
editor@thegospeltruth.org

Utakatifu kwa Bwana